**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA WAZIRI MKUU-TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

SHULE YA SEKONDARI PUNI,
S.L.P 835,
**SHINYANGA.**
……-…..-20….

Mawasiliano
Mkuu wa Shule: 0758144299/ 0621093022
Makamu Mkuu wa Shule: 0769332806
Mwalimu wa Malezi: 0759519035
Mzazi/ Mlezi wa Mwanafunzi: ______________________________________________
S.L.P:____________
_________________

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI PUNI HALMASHAURI YA WILAYA SHINYANGA, MWAKA …………..**

## 1.0. UTANGULIZI

Ninafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha tano katika shule hii, mwaka 2026. Shule iko umbali wa mita 900 toka barabara kuu itokayo Tinde kwenda Kahama, kijiji cha Puni, kata ya Puni, halmashauri ya wilaya ya Shinyanga. Nauli ya Hiace toka Tinde ni 1500/= na kutoka Kahama ni 4,000/=

Muhula wa masomo utaanza tarehe ……………….. kama itakavyotangazwa na Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI.

## 2.0. Mambo muhimu ya kuzingatia:-

## 2.1. SARE YA SHULE (DARASANI)

### 2.1.1. WASICHANA

i. Sketi mbili rangi ya bluu mkolezo (dark blue), belti iwe na upana wa nchi $2\frac{1}{2}$ mpaka nchi 3, rinda moja pana nyuma na mbele (nchi 8) na marinda mawili madogo kushoto na mawili kulia. Iwe ndefu iguse kifundo cha mguu (ankle) isiyobana mwili.
ii. Mashati mawili (2) rangi ya bluu bahari, mikono mirefu kila shati liwe na mfuko mmoja kifuani upande wa kushoto.
iii. Tai moja ndefu rangi ya bluu mkolezo yenye mistari mitatu katikati. (kwa wasio waislamu)
iv. Viatu vya ngozi nyeusi vya kufunika vya kufunga kwa gidamu (**kamba**), visiwe na urembo wala visiwe virefu (visiwe boot).
v. Soksi nyeupe jozi mbili (2) ndefu.
vi. Nywele fupi (zisizidi Sm1 moja) au kusuka msuko wa mkono kutoka mbele kwenda nyuma makonga matano.
vii. Sweta rangi ya blue bahari (light blue).
viii. T-shirt ya rangi ya njano, yenye nembo ya shule. (15,000/=)
ix. Hijabu nyeupe kwa mabinti wa kiislamu (ifunike viwiko).

### 2.1.2. WAVULANA

i. Suruali (2) za rangi ya bluu mkolezo (dark blue), ushonaji-mfuko mmoja wa nyuma wa ndani, isiwe fupi na isiyobana miguuni.
ii. Mashati mawili (2) ya bluu bahari, mikono mirefu, yenye mfuko mmoja kifuani kushoto.
iii. Tai ndefu, (1), moja rangi ya blue mkolezo (dark blue), yenye mistari mitatu katikati.
x. Viatu vya ngozi vyeusi vya kufunika vya kufunga kwa gidamu (**kamba**), visiwe na urembo wala visiwe virefu (visiwe boot).
iv. Soksi nyeusi, zisiwe na urembo. jozi 2.
v. Mkanda wa suruali mweusi usiwe na pini kubwa wala mpana sana (usizidi Sm5).
vi. Nywele fupi. (zisidi Sm moja (1).
vii. Sweta rangi ya blue bahari (light blue).
viii. T-shirt ya rangi ya njano, yenye nembo ya shule. (15,000/=)

2.2.0. SARE YA KUSHINDIA

2.2.1. WASICHANA

Nguo za kushindia (shamba dress) rangi ya blue mkolezo), kitambaa cha suti, mshono wa solo, urefu mpaka kwenye kifundo cha mguu, mikono mirefu/mifupi. Pia inapatikana shuleni kwa bei ya shilingi 30,000/= kwa atakayehitaji

2.2.2. WAVULANA

Tshirt ya bluu (Blue) na suruali nyeusi. (15,000)

**2.3.0. SAREZAMICHEZO**

i. Tracksuit rangi nyeusi kwa wote.
ii. Tshirt nyeupe ya Adidas au Nike mikono mirefu au mifupi. Pia zinapatikana shuleni kwa bei ya shilingi 15,000/= kwa atakayehitaji
iii. Raba au njumu na soksi vya rangi yoyote.

**Zingatia:** Kwa mwanafunzi aliyekuwa mwanachama wa skauti na anapenda kuendelea aje na sare za skauti.

3.0. Michango ya Shule

| **NA** | **AINA YA MCHANGO** | **KIASI** |
|---|---|---|
| 1 | Mchango wa uendeshaji wa shule | 65,000/= |
| 2 | Tahadhari | 5,000 |
| 3 | Nembo | 5,000/= |
| 4 | Kitambulisho | 5,000/= |
| **JUMLA** | | **80,000/=** |

- Fedha hizo zilipwe kwenye Akaunti ya shule Na. 0150849746300, yenye jina la **PUNI SECONDARY SCHOOL CAPITATION AC** katika Benki ya CRDB (Tafadhali andika jina la mwanafunzi kwenye pay in slip).
- **Zingatia**: Kila mzazi/mlezi amkatie mwanae bima ya afya ya NHIF ya Tsh. 50,400/= kwa mwaka au alipe shuleni kiasi cha Tsh. 50,400/= taslimu na mwanafunzi mwenye umri wa miaka 18+ awe na namba ya utambulisho wa taifa (NIDA) kwa ajili ya bima hiyo na kama hana namba ya NIDA fedha haitopokelewa. Kwa mwanafunzi ambaye tayari ana bima ya NHIF aje na kadi na mchango wa Tsh. 50,400/= **hautamhusu.**

4.0. Mahitaji muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuleta shuleni (pia yanapatikana shuleni) ni kama ifuatavyo:

i. Ream ya karatasi 2 (kwa mwaka) @ 12,000/=,
ii. Vitabu vya masomo ya taasusi husika (angalia orodha ya vitabu iliyoambatanishwa).
iii. Godoro futi 3 aina yoyote (Malaika 35,000/=; Victoria 45,000/=; Superbanco 58,000/=; Tanform 80,000/=) kwa atakayehitaji
iv. Mashuka manne (4); 2 meupe na 2 blue tu bila maua @ 12,000/=, mto 1@ 5,000/= (mto sio lazima), chandarua 1 round na rangi yoyote @ 10,000/=, kwa atakayehitaji
v. Vyombo vya chakula (sahani 1 @ 1,000/=; bakuli 1 @ 1,000/=; kijiko 1 @ 500/= na kikombe1 @500/=), jumla 3,000/=,kwa atakayehitaji
vi. Ndoo mbili ndogo zenye mifuniko @ 5,000/=, nakwa atakayehitaji
vii. Fyekeo/kwanja moja 3,500/=, jembe moja, na mpini wake @ 7,000/=; na ufagio wa nje (3500/=) kwa HGK kwa mzazi/mlezi atakayehitaji
viii. Reki moja na mpini 10,000/=; mfagio wa ndani mmoja 3,500/= na brush ngumu (3500/=) kwa HGL kwa mzazi/mlezi atakayehitaji
ix. Folder file moja na kamba yake (file tag) kwa wote

5.0. Viambatanisho na Fomu Muhimu:

i. Fomu ya uchunguzi wa afya (medical examination form) ambayo itajazwa na mganga wa hospitali ya serikali.
ii. Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi/mkataba wa kutoshiriki katika mgomo, fujo na makosa ya jinai,
iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni, kulipa michango na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule,
iv. Nakata ya matokeo ya kidato cha nne (Form four result slip) na nakala ya cheti cha kuzaliwa (birth certificate)
v. Picha nne (4) za wazazi/walezi na ndugu wa karibu wa mwanfunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na namba zao za simu, na

- **Tafadhali soma kwa makini maelezo/ maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.**

**MACHAGE M. MAGINGA**
**MKUU WA SHULE**

## 6.0. SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

**6.1 Sheria na Kanuni za Shule**

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku (preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; nesi wa shule na mwalimu wa malezi.
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.
xii. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa kama simu ya mkononi, pasi (ya umeme au mkaa), radio ama kifaa chochote cha mziki.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**
- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**

- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).

**6.2. Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka nywele kwa mtindo ulioelekezwa kwa wasichana.
vii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
viii. Uvutaji wa sigara;
ix. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
x. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xi. Kusababisha mimba;
xii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiii. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xiv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule; Kudharau Bendera ya Taifa;
xv. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xvi. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi
xvii. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au na mtu yoyote yule.
xviii. Kutembelea nyumba za watumishi bila kibali maalum.
xix. Kuingia ofisi za watumishi bila kibali maalum.
xx. Kushiriki/Kusaidia kutoa mimba
xxi. Kumtesa mwanafunzi mwenzake/kumdhalilisha na kumnyima raha.
xxii. Kugomea adhabu/kukataa adhabu.
xxiii. Kuendesha biashara ya aina yoyote shuleni.
xxiv. Kukaribisha wageni bila idhini ya uongozi wa shule.
xxv. Kulala nje ya shule bila ruhusa.

xxvi. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma/mwanafunzi mwenzake.

xxvii. Kutumia vipodozi vya kuchubua ngozi (Cosmetics) kwani ni hatari kwa afya.

xxviii. Kutofanya usafi katika majengo muhimu shuleni kama mabwenini, darasani, vyooni, bwaloni, ikiwemo kufagia, kupiga deki, kuondoa buibui popote zitakapo onekana na usafi wa mazingira kwa ujumla. Kutunza na kuboresha mazingira ya shule kama kupanda miti na maua kwenye ndoo.

xxix. Ni lazima wanafunzi wote wavae sare ya shule (full uniform) wakati wote wa :-

a) Masomo darasani/siku ya vilabu vya masomo.

b) Wanapotoka nje kwa shughuli za kishule.

c) Mihadhara ya shule ikiwemo school baraza.

d) Wanapoenda hospitali

e) Kufanya kazi za nje "Extra- Curricular activities" wavae sare za kazi.

f) Wanapoenda Kanisani/ msikitini.

g) Wanaposafiri kuja shuleni/ kwenda makwao.

h) Tracksuit ivaliwe wakati wa preparation ya usiku na sio wakati wowote.

i) Nguo za michezo zivaliwe wakati wa michezo tuu. Nguo za aina yoyote za nyumbani hazirusiwi kuvaliwa wakati wa michezo au kazi za nje, hivyo mwanafunzi asije na nguo za nyumbani.

xxx. Mwanafunzi haruhusiwi kutoka nje ya mipaka ya shule wakati wa masomo/mapumziko, isipokuwa kwa ruhusa maalum.

- **Zingatia: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao).Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZILIZOPO JUU.**

## 7.0. OFISI YA RAIS-TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
## SHULE YA SEKONDARI PUNI, SHINYANGA

**MAELEZO BINAFSI / MKATABA WA MWANAFUNZI**

A. JINA LA MWANAFUNZI…………………………………………………..
KIDATO………………………….. MWAKA……………………………….
TAREHE YA KUZALIWA………………………MTAA /KIJIJI………………
KATA……………………………………………………………….
TARAFA……………………………………………………………
WIALAYA…………………………………………………………
MKOA………………………………………………………..

B. JINA LA
BABA…………………………………………………hai/amefariki/haijulikani

C. JINA LA MAMA
……………………………………………...hai/amefariki/haijulikani

D. Mimi (jina kamili)………………………………………………….mwanafunzi wa kidato cha………tahasusi ya…………..kwa akili yangu timamu nimekubaliana na mkataba wa kutoshiriki katika mgomo, fujo na makosa ya jinai.

E. SAHIHI………………………………………TAREHE……………………………

**FOMU YA MKATABA WA MZAZI/MLEZI**

A. JINA KAMILI LA MZAZI/MLEZI……………………………………………………
B. MZAZI/MLEZI WA (Jina la mwanafunzi)……………………………………
C. ANUANI/ANAKOISHI…………………………………………………………
D. Mimi (Jina la mzazi/mlezi)……………………………………………………nakiri kukubaliana na sharia kanuni, kulipa ada, michango na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule ya sekondari Puni.
**E.** SAHIHI…………………………………………..TAREHE……………………

**8.0. MAJINA NA PICHA ZA NDUGU/JAMAA WANNE AMBAO SHULE INAWEZA KUWASILIANA NAO NA WANAOWEZA KUMTEMBELEA MWANAFUNZI SHULENI.**

Jina la mwanafunzi………………………………………kidato……tahasusi………..mwaka......

i. JINA……………………………………………………….ANUANI…………………
…

SIMU………………………………UHUSIANO…………………………

ii. JINA……………………………………………………….ANUANI…………………

SIMU……………………………UHUSIANO…………………………………………….

iii. JINA……………………………………………………….ANUANI…………………

SIMU…………………………………UHUSIANO…………………………………

**9.0. PRESIDENT'S OFFICE – REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT,**

**PUNI SECONDARY SCHOOL,**

**P.O.BOX 835,**

**SHINYANGA.**

**REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION**

**To the medical officer,**

________________________

________________________

**RE:**_____________________________________________________________________________

_____________

**Please examine the above named if she is physically and mentally fit for studies in this school. The examination should include/ the following categories:-**

**1. (a) Eyes**_______________________________________________

**(b)Ears**__________________________________________________________________________

__________________________________

**(c) Chest…………………………**_______________________________________________

**(d) Spleen**_____________________________________________

**(e) Abdomen**__________________________________________

**(f) Urine…………………………**_______________________________________________

**(g) Stool examination……………………………**

**(h) Blood**______________________________________________

**(i) Skin………………………………**_______________________________________________

**(j) Tuberculosis……………………………….**

**(k) Speech**_____________________________________________

**(l) Epilepsy**____________________________________________

**(m) Limbs (i.e. has muscle weakness)………………………..**

**2. Pregnancy (For girls)__________________________________________**

**3. Other serious diseases e.g. diabetes, anemia and rheumatism……………………………………….____________________**

**4. Any additional information e.g. physical defects or impairments, injections, chronic or family diseases, etc……………………………………______________________________**

**MEDICAL CERTIFICATE**

**(To be completed by a Government Medical Officer)**

**I have examined the named and consider that she is physically fit/unfit for full time studies in this school.**

**NAME:___________________SIGNATURE____________STATION_______________**

**Designation……………………. Office**

**Stamp________________________**

## 10.0. SARE ZA SHULE

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
|  |  |  |  |  |
| **SWEATER (FOR ALL)** | **SKIRT (FOR GIRLS)** | **TIE (FOR ALL)** | **SHAMBA DRESS (FOR GIRLS)** | **TRACKSUIT (FOR ALL)** |
|  |  |  |  |  |
| **TRAUSER (FOR BOYS)** | **SHIRT (FOR ALL)** | **OFICIAL TSHIRT (FOR ALL)** | **SHAMBA TSHIRT (FOR BOYS)** | **SPORTS TSHIRT (FOR ALL)** |

## 11.0. ORODHA YA VITABU

### 11.1. PHYSICS

I. Physics for Adv. Level secondary schools. Student’s book form 5 – TIE

II. Physics for Adv. Level secondary schools. Student’s book form 6 – TIE

### 11.5. GEOGRAPHY

I. Pritchard M, John (1971) Practical Geography for Africa.

II. DT. Msabila (2007) A Comprensive Approach to Physical Geography for Secondary Schools.

III. Msabila, DT (2000) An Intergrated Focal Regional Study onHuman and Economic Geography.

### 11.7. KISWAHILI

I. Kamusi ya Kiswahili – Longhorn

II. Kiswahili shule za sekondari, kitabu cha mwanafunzi kidato cha 5 & 6– Fasihi. – TIE

III. Kiswahili shule za sekondari, kitabu cha mwanafunzi kidato cha 5 & 6– Fasihi. – Lugha na sarufi TIE

IV. Historia ya Tanzania na Maadili. Form Five. TIE. Kwa wote

V. Academic Communication. Form Five. TIE. Kwa wote

VI. DUNIA UWANJA WA FUJO, cha Euphrase Kezilahabi

VII. UA LA FARAJA cha W.E. Mkufya

VIII. MIRATHI YA HATARI cha C.G. Mung’ong’o

IX. WASIFU WA SITI BINTI SAADI cha Shaaban Robert

X. Mukwawa wa Uhehe cha Nyambari Nyangwine

XI. Shujaa Milambo cha Emmanuel Mbogo

XII. Usaliti Mjini cha Francis Imbuga

XIII. Fumbo linaloelea cha Nyambari Nyangwine

XIV. Malenga wa Ziwa Kuu cha Wallah bin Wallah

XV. Andamo, Msafiri Safarini, cha Mohammed K. Ghassani

XVI. Wosia wa Baba, cha Ahmed Mohamed Amanzy.

### 11.8. ENGLISH LANGUAGE

I. Ibsen, H (1967). An Enemy of the People Nairobi. Heinemen Education Books Ltd.

II. AN ANIMAL FARM. By George Orwell

III. CHASING THE LEOPARD FINDING THE LION. By Julie Wakemqn-Linn
IV. THE OPPORTUNIST ELITE. By Nyambari Nyangwine
V. THE HORIZON UNVEILED. By Fellows Mwaisela
VI. THE GOVERNMENT INSPECTOR. By Nikolai V. Gogol
VII. A TASTE OF HEAVEN. By Farouk Topan
VIII. SUMMONS: Poems from Tanzania. By Richard S. Mabala et al
IX. POETS OF AFRICA: Lament of the Silent & Other Poems